

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Kilimanjaro imekuwa ikipokea malalamiko mbalimbali kutoka kwa wawekezaji ndani ya Mkoa hususani Wilaya ya Hai. Malalamiko hayo yamelenga kwenye taratibu zinazotumika na viongozi katika kushughulikia mapungufu yanayojitekeza kwa wawekezaji wa mashamba makubwa ya vyama vya ushirika.

Kutokana na hali hiyo uongozi wa Mkoa umelazimika kuitisha vikao kadhaa ili kujadili namna sahihi ya kutatua changamoto hizo. Katika kikao cha tarehe 06/09/2018 kilichohusisha wawakilishi wa wawekezaji, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, Wataalamu kutoka Sekretariat ya Mkoa na Uongozi wa Wilaya ya Hai tulijadili mambo kadhaa ikiwa ni pamoja na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa mkataba wa pango kati ya N.G Emmanuels na Chama cha Ushirika Nshara.

Katika majadiliano hayo ilibainika kuwa Chama cha Ushirika Nshara kina mkataba wa pango kwa miaka 20 na kampuni ya uwekezaji G.N. Emmanuels Limited toka mwaka 2012 hadi 2032. Hata hivyo wakati wa utekelezaji wa mkataba huo imeonekana mnamo mwaka 2014 G.N Emmanuels aliiharikabisha kampuni ya African Vegetables Limited (AVL) kuwekeza katika ekari 5 za shamba hilo bila kupata ridhaa kutoka kwa mwenye shamba (Nshara AMCOS). Kwa kupitia hekari 5 ambazo AVL anazitumia kuwekeza. AVL aliomba leseni ya unafuu wa kodi kwenye mamlaka ya EPZA na akapewa leseni hiyo kinyume cha sheria ya EPZA Na.11 ya mwaka 2002. Hivyo amekuwa halipii kodi kwa bidhaa anazozalisha kwenye kiwanda alichojenga katika shamba la Makuru Estate.

Kufuatia utata ulioainishwa hapo juu imebainika kuwa kuna mapungufu yanayotokana na kutozingatia sheria na kanuni katika utekelezaji wa mkataba wa pango kati ya N.G Emmanuels na Chama cha Ushirika Nshara kufuatia hali hiyo imebainika kuwa;

- I. Taratibu zilizotumika na kampuni ya AVL kuingia katika shamba la Makuru Estate linalomilikiwa na chama cha ushirika Nshara wakati mpangaji kwenye shamba hilo ni kampuni ya G.N. Emmanuels hazikuwa sahihi. Hivyo kampuni ya AVL imewekeza katika shamba la

Makuru Estate kinyume na taratibu. Mkataba wa pango umeweka wazi kuwa kama mpangaji atakuwa na nia ya kumpangisha mtu mwingine shamba hilo basi ni sharti apate kibali kutoka kwa mpangishaji, jambo ambalo halikufanyika.

- II. Ubia iliopo kati ya kampuni ya G.N. Emmanuels na kampuni ya AVL ni kwamba wakati kampuni ya AVL inaanzishwa mwaka 2014 kampuni ya G.N. Emmanuels ni mojawapo ya wanahisa wa kwanza walioorodheshwa kwenye vitabu kuwa wanaochukua hisa zilizopelekea AVL kupewa cheti cha usajili (Certificate of Incorporation).
- III. Kampuni ya AVL imesajiliwa EPZA kwa kutumia ardhi ambayo si yake hivyo taratibu zilizotumika zilikiuka Sheria ya EPZA Na.11 ya mwaka 2002 ambayo inatoa sharti la mtu anayeomba leseni ya msamaha wa kodi awe na ardhi. Inaelekeza EPZA haikujiridhisha na taratibu zinazostahili kuzingatiwa na mwekezaji kabla ya kutoa leseni kwa AVL. Aidha, inaelekea pia Wanasheria wa Mwekezaji hawakujiridhisha ipasavyo wakati wa kumshauri mteja wao kuhusu taratibu za upatikanaji wa leseni inayotolewa na EPZA. Hali hii ilipelekea EPZA kutangaza ardhi hiyo kuwa eneo la EPZA kwa mujibu wa kifungu cha 3(1) cha Sheria ya EPZA, hivyo kwa kuwa AVL alitumia njia zisizo sahihi kupata leseni hivyo anastahili kufutiwa leseni kwa mujibu wa kifungu cha 7(1) cha Sheria ya EPZA.

Kwenye kikao cha tarehe 09/09/2018 kilichowashilikisha wawekezaji, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri, Wenyeviti wa Halmashauri, Wawakilishi wa vyama vya Ushirika na Wataalamu kutoka Sekretariat ya Mkoa. Kikao hicho kilizingatia mambo mbalimbali yaliyojitokeza katika maeneo ya uwekezaji na baada ya mjadala mrefu iliazimiwa ifuatavyo:-

- Serikali inahimiza wawekezaji wafuate taratibu, sheria na miongozo ya wawekezaji.
- Wawekezaji ni sharti wajenge mahusiano mazuri kati ya wazawa na wenye shamba. Hii itasaidia kuwa na mazingira bora ya uwekezaji.
- Wawekezaji wanao wajibu wa kuwalipa wafanyakazi wanaofanya kwenye mashamba yao mishahara unaolingana na kima cha chini cha kwenye sekta binafsi.
- Wawekezaji wawe na ubia na Chama cha Ushirika au wenye shamba ili wamiliki wa mashamba waweze kujua namna ya uendesaji wa masuala ya Ushirika.
- Wawekezaji wanaowajibu wa kuwa na mahusiano mazuri na uongozi uliopo kwenye maeneo yao ya uwekezaji.

HITIMISHO.

Ni vema wawekezaji wakatambua kuwa wakija kuwekeza katika taifa letu wanastahili kuzingatia sheria za nchi na siyo kizikiuka.

DKT. ANNA E. MGHWIRA
MKUU WA MKOA
KILIMANJARO
10/09/2018